

**LEARNING BY EAR 2009**  
**Economics – 10<sup>th</sup> episode**

**SUCCEEDING IN THE BUSINESS WORLD**

**Series:** “THE STORY OF TWO YOUNG PEOPLE, WHOSE  
SUCCESS STEMS FROM THEIR POCKET MONEY”

**Author:** Frédéric GAKPARA

**Editors:** Yann Durand and Sandrine Blanchard

**Translator:** Anne Thomas

**Kisuaheli:** Eic Ponda

**TENTH EPISODE:** “At the World Trade Fair”.

**Characters:** **Jane** (*21 years old, CEO of AOOT*)  
**John** (*21 years old, in charge of conditioning AOOT*)  
**1<sup>st</sup> Customer** (*49-year-old man*)  
**2<sup>nd</sup> Customer** (*56-year-old woman*)  
**Organizer** (*39-year-old man*)  
**Journalist** (*31-year-old man*)  
**President of Organizing Committee – PCO** (*woman, 63 years old*)  
**President of the jury – P JURY** (*man, 67 years old*)  
**Exhibitors, Hosts, Audience...**

**NARRATOR:**

Hujambo mpenzi msikilizaji wa Deutsche Welle na karibu kwa makala yetu ya 10 na mwisho ya Learning By Ear kuhusu masuala ya Uchumi. Hii ni hadithi ya Vijana wawili Mapacha ambao kwa kujikakamua kwao kubania matumizi wameza kufika upeo mkubwa kiuchumi. Jane sasa amerejea kutoka safari yake ya mataifa Ulaya akiwa na ujuzi mkubwa wa kibiashara baada ya kupata mafunzo na vidokezo kutoka kwa Baba mdogo Sami kabla ya kuelekea Switzerland huku Kampuni yake ikiendelea kuimarika. Sasa ni mkurugenzi mkuu wa kampuni yao ilhali John amechukua jukumu la kuwa meneja wa bidhaa na mauzo. Licha ya tofauti kuzuka baina yao ya hivi majuzi, Jane anakubali kuandamana na Kaka yake kuhudhuria maonyesho ya kimataifa ya kibiashara. Ndio mwanzo maonyesho hayo yamefungua, milango na John anashughulikia kibanda chao huku naye Jane akizungumza na wateja...

**Scene 1, AT JANE'S STAND**

JANE, JOHN, 1<sup>st</sup> CUSTOMER, 2<sup>nd</sup> CUSTOMER, AN ORGANISER, THE JOURNALIST...

**ATMO:** *Crowd of visitors to the salon.*

1. **Jane:** (*Very fast*)  
Habari Bw ! Karibu Biskuti na peremende kutoka Africa!Kibanda chetu kiko pale! Kuna bidhaa nyingi tu asili zinazotengenezwa kutokana na Njugu.Pia tuna siagi na matunda yaliyokaushwa.
  
2. **1<sup>st</sup> Customer:** (*With an English accent*)  
Samahani?
  
3. **Jane:** Matunda yanatayarishwa kwa ustadi kabisa .Karibu uonje matunda hayo,kibanda chetu kiko pale mbele kidogo...
  
4. **1<sup>st</sup> Customer:** Unasema unatoka Africa?
  
5. **Jane:** Ndio,! Kampuni yetu inaitwa “Appetizers of the Tropics” Kibanda ndicho hiki hapa!(*To John*)  
John,Mpe maembe ya kukausha huyu Mzee aonje.  
(*to the customer*)  
Tayari tunayauza katika soko la Ujerumani, Switzerland ,Qatar, Saudia, Brazil na mataifa mengineyo.

6. **1<sup>st</sup> Customer:** Kweli?  
(*He tastes*)  
Uum...ni matamu sana. Mnayatayarisha vipi?
7. **Jane:** Kwa kutumia siri tuliyopewa na Bibi yetu!  
(*Laughing*)  
Pia tuna njugu , Baskuti na peremende aina ya **Lollipop**. Filosofia yetu ni kuitangaza Africa.
8. **1<sup>st</sup> Customer:** Nimefurahishwa sana na juhudi zenu.Ni wazo zuri sana. Ningetaka sana kushirikiana nanyi. Hii ni kadi yangu ya biashara. Mimi pia niko katika sekta ya biashara ya vyakula.Nauza vyakula vya aina mbali mbali katika miji mingi nchini Canada.Ningependa sana kujaribu bidhaa zenu.Unaweza kunipigia simu wakati wowote ili tuweze kuzungumza zaidi...
9. **Jane:** Nitachukua hiii siagi nikajaribu. Kwaherini tuonane baadaye.
10. **1<sup>st</sup> Customer:** Asante sana!
11. **John:** Jane, peremende za **Lollipo** zimeisha.
12. **Jane:** Oh no! Ohhhoo, sawa, usijali.... Najua tutafanya nini...! Shughuli itaendelea tu kama

kawaida! Habari Mama! Karibu uonje Siagi tamu na matunda ya kukaushwa kutoka Afica?

13. **2<sup>nd</sup> Customer:** Ni matunda gani hayo?
14. **Jane:** Ndizi, Maembe, Papai, .... Karibu uonje! Tumeyakausha ili kudumisha ladha yake asili...
15. **2<sup>nd</sup> Customer:** Ni matamu ! Mkubwa wenu yuko wapi?
16. **Jane:** Mimi hapa ndio mkurugenzi mkuu wa kampuni yetu.
17. **2<sup>nd</sup> Customer:** Una hakika? Lakini waonekana mdogo sana!
18. **Jane:** *(Laughing)*  
Ndio, sisi bado wadogo sana,... wadogo lakini tumejitolea!
19. **2<sup>nd</sup> Customer:** Nafurahi kusikia hivyo! Tunaweza kukutana badaye Hotelini mwangu ili tuzungumzie uwezekano wa kuanzisha ushirikiano? Mimi nasimamia kampuni ya vyakula ya “FOOD SPACE” nchini Marekani na Canada. Hii hapa anuani ya Hoteli.

20. **Jane:** Shukrani sana Mama!. Chukua Ndizi, **Jam** na hizi baksuti, ni nzuri sana kwa chai
21. **2<sup>nd</sup> Customer:** Asanteni sana. Kwa ukarimu wako Bi.....?
22. **Jane:** Jane!
23. **2<sup>nd</sup> Customer:** Asante Bi Jane! Nipigie simu ningependa sana kuzungumza nawe.
24. **Jane:** Usiwe na shaka Mama! , Nitakupigia simu baadaye, Kwaheri.!
25. **John:** (admiringly)  
Kweli nimeamini!
26. **Jane:** Kaka lazima uwe ngangari ndio uweze kufaulu katika biashara!
27. **An organizer:** Hallo, Bi...!
28. **Jane:** Hello, naweza kukusaidia?
29. **Organizer:** Mimi ni afisa msimamizi wa maonyesho haya. Nimepata habari kutoka kwa baadhi ya wenye vibanda kwamba mnawashawashi wateja mbele ya vibanda vyao, ni kweli?

- 30. Jane:** Ohh! Kibanda gani, mimi nimekuwa nikizunguka tu katika sehemu zilizotengwa watu kupitia, na sijui unachosema...
- 31. Organizer:** Tafadhali mubakie katika kibanda chenu... sawa? Maonyesho haya ni ya watu wote na tunalinda haki za kila mmoja. Nikisikia tena malalamishi hayo nitakifunga kibanda hiki!
- 32. Jane:** Sawa nimekuelewa Bw. (*To a passer by*) Habari gani! Pita ndani ujionee matunda ya Africa! Hapa tuna matunda mazuri na Peremende zilizotengenezwa kutokana na Njugu karanga.
- 33. Journalist:** Kutokana na nini?
- 34. Jane:** Kutokana na Njugu!....! Kampuni yetu ni nambari moja barani Africa kwa biashara ya vyakula. Tayari tumeweza kuyashawishi mataifa kadhaa katika mabara mengi kuhusu ubora wa bidhaa zetu .Na zaidi ni matunda asilia kabisa!
- 35. Journalist:** Naweza kuonja ?
- 36. Jane:** Unaweza kuonja !Hizi hapa ni Baskuti zilizotengenezwa kutokana na unga wa

Njugu.Zina ladha ya nazi na hazina mafuta mengi, ni asilimia 5 pekee na hazina sukari. Unazisikiaje!

- 37. Journalist:** Ummm, ummm! ummm! Ni tamu sana!Mimi ni muandishi wa habari kutoka Deutsche Welle. Ugependa tufanye mahojiano kuhusu bidha zenu?Nitaka kuangazia kibanda chenu.
- 38. Jane:** Niko tayari! twendelee!
- 39. Journalist:** Kwanza kabisa unaweza kujitambulisha kwa wasikilizaji wetu!
- 40. Jane:** Jina langu ni Jane....
- 41. ATMO:** *Jane's voice is drowned by the sound of the trade fair??...*
- 42. Jane:** ..... Miblemi, Mimi ni mkurugenzi mkuu wa kampuni ya “Appetizers of The Tropics”.
- NARRATOR:** Jane ametumia ujuzi wake kuwavutia wateja wengi katika kibanda chache.Amejuana na watu wengi, kukutana na wafanyi biashara mbali mbali na hata kutia sahihi mikataba ya kibiashara.Siku mbili kabla ya kumalizika kwa maonyesho hayo, kunaandaliwa karamu ya watu mashuhuri...



## Scene 2, AT THE VIP CEREMONY

PERSIDENT OF THE ORGANIZING COMMITTEE (PCO), PRESIDENT OF THE JURY (P JURY) JANE, JOHN, EXHIBITORS, HOSTS, AUDIENCE

43. **ATMO:** *festive atmosphere. Announcements through the loudspeakers*
44. **PCO:** ...Leo tunafunga milango ya maonyesho haya ya kimataifa . Cha kufurahisha ni kwamba Bara la Africa linaendelea kushangaza wengi kutokana na juhudi za kuimarisha bidhaa zake. Na tuzo zetu mbili za kwanza zinaiendea kampuni kutoka Africa, "***Appetizers of the Tropics***"....
45. **ATMO:** *Cries of joy from Jane's delegation, hearty applause...*
46. **PCO:** Kampuni ya "Appetizers of the Tropics" imeshinda tuzo mbili na kisha tuzo jingine la kuwa na wafanyi biashara chipukizi !
47. **ATMO:** *More cries of joy and applause...*

- 48. PCO:** Ushindi wa mapacha, Kijana na msichana, ni wafanyibiashara chipukizi. Na licha ya umri wao mdogo wa miaka 21, wamefaulu kuanzisha kampuni kubwa na kisasa kwa kujitolea kwao kubania matumizi. Ni hadithi yenye mwanzo wa kuhuzunisha na ndoto iliyotimia ambayo tungependa kushereheka mwaka huu. Naamini huu ni mfano mzuri wa kuigwa na vijana kote ulimwenguni. Bi Jane na Bw John tafadhali muje hapa mbele jukwaani! Mabibi na Mabwana na sasa ni furaha yangu kuwajusheni kwa wasimamizi wa kampuni ya “The Appetizers of the Tropics”! Bi Jane na Bw John!
- 49. ATMO:** *Crowd applauds, fanfare, shouts ...*
- 50. PCO:** Tafadhali Rais wa shirikisho la maonyesho haya ya kimataifa sasa unaweza kuwakabidhi tuzo zao!
- 51. ATMO:** *Silence in the room...*
- 52. P Jury:** Kwa niaba ya jopo la majaji katika maonyesho haya ya kimataifa makala ya 32<sup>nd</sup> ninamtuza Bi Jane, mkurugenzi wa “Appetizers of the Tropics”, tuzo la kibanda

bora na pia wafanyi biashara chipukizi  
kabisa.

**53. ATMO:**

*Thundering applause, shouts...*

**54. PCO:**

Tafadhali.. tafadhali.... Bi Jane ungependa  
kusema machache?

**55. ATMO:**

*Silence in the room...*

**56. Jane:**

*(Emotional)*

Mi...mi ... .. Ni kama ... .! Nataka kutoa  
shukurani kwa kila mmoja wenu.....

Tulianzisha kampuni hii na kiasi kidogo chini  
ya dola sita. Wakati tulipoanza, hatukujua  
tungeweza kufika kiwango hiki. Kwa mara  
nyingine natoa shukurani zangu kwa jopo la  
majaji. Pia nawashukuru shirika la wafanyi  
biashara Barani Africa, ambalo limetusaidia  
kufika hapa. Ningependa kutoa heshima  
zangu na kuelekeza ushindi huu kwa Bibi  
yangu ambaye ametusaidia kufika mahali  
tulipofika hivi sasa. Asanteni sana na sasa  
nampa nafasi Kaka yangu John

**57. John:**

*(Clearing his throat)*

Poleni... Namshukuru sana Dada yangu  
Jane,... ametuongoza vyema tangu

mwanzoni. Nikutokana na juhudi zake ndio leo tuko hapa. (*To Jane*) Asante sana Jane, na naelekeza sifa zote za kuwa na kibanda bora kwako Dada, Unastahili sifa hizo!

**58. ATMO:** *Applause in the crowd, fanfare ...*

**NARRATOR:** Wakitiririkwa na machozi kwa furaha Jane na John wanakumbatiana, huku waandishi wa habari wa kimataifa waking'ang'ana kuwapiga picha .Hadithi ya ufanisi wao sasa umewachochea wateja wengi zaidi kuzuru kibanda chao. Tunakutana nao tena baadaye katika mkahawa wa kampuni yao wakionekana wachovu baada ya shamra shamra za maonyesho hayo...

## Scene 2, AT THE HOTEL CAFÉ

JANE AND JOHN...

**59. ATMO:** *Soft music in the background. Sounds of mugs and spoons.*

**60. John:** Nimekuheshimu sana Jane!

**61. Jane:** Asante ! Pia ulinisaidia sana kunipa moyo wa ujasiri kuendelea na biashara hii!

**62. John:**

Ningependa kuona machozi ya furaha yakitiririka kila siku. Najua umenisamehe Jane, na natamani ningeweza kukufanya usahau yote yaliyopita. Yote niliyokukosea Dada yangu na hata machungu uliyokuwa nayo ukiwa Hospitalini.

**63. Jane:**

Tusahau hayo yaliyopita. Sisi sote hujifunza kutokana na makosa yetu. Sasa tunapasa kusherehekea ufanisi wetu, kilicho muhimu ni kuelekeza juhudi zaidi kudumisha hadhi tuliyotunukiwa na kuimarisha biashara hii kwa heshima ya bara zima la Africa na Ulimwengu kwa jumla. Kampuni hii ya "Appetizers of the Tropics" sio kampuni yetu pekee bali mali ya Bara la Africa "**sura ya Africa**". Ni dhihirisho la heshima na kielelezo kwa wafanyi biashara chipukizi katika kanda hii.

**64. John:**

Shukrani nyingi kwa upendo wako kwangu. Tabia yangu ingelinifanya kushuka ngazi katika kampuni yetu lakini kwa sababu yako, nimekuwa mtu mwenye majukumu na nitafanya kila juhudi kadri ya uwezo wangu kufanikisha na kukuza biashara hii, kwa ajili yako na Africa nzima

**65. Jane:** Tunyoshe glasi zetu juu, kutoa pongezi kwa vijana wa Africa, vijana ambao kwa juhudi zao wametimiza ndoto na kuletea sifa bara hili....

**66. ATMO:** *They toast.*

**67. John:** Na sasa, tuingilia maisha yako Jane, ni mvulana gani.....

**68. Jane:** *(she interrupts him)*  
Nini !? Hapana hapana , John sasa sitaki uingilie maisha yangu?

**69. ATMO:** *They both laugh heartily...*

**NARRATOR:** Na hivyo ndivyo John na Jane walivyoweza kufika upeo wa biashara baada ya mwanzo mgumu na changamoto nyingi katika kubania matumizi yao. Sasa mapacha hawa wametunukiwa jukumu la kuwa kielelezo cha maendeleo, kuwa wanyenyekevu na mfano bora kwa vijana wengine kufanikisha ndoto zao.

**70. Closing soundtrack to be left running after the outro and brought up**

**NARRATOR:** Tumefika mwisho wa mfululizo wa hadithi hii ya Mapacha wawili waliofanikiwa kibiashara kutokana na

juhudi zao za kubania matumizi. Ni mchezo wa Learning By Ear unaotayarishwa na Deutsche Welle ulioandikwa na.

**Frédéric Gakpara!**

Kutiwa sauti na :

Mhariri alikuwa : ***Yann Durand and Sandrine Blanchard***

Na umtafsiriwa na : ***Anne Thomas Na Eric Ponda***

Fundi wa mitambo:

Msimamizi :

Kumbuka ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa **dw-world.de/l b e**.

Pia ukiwa na maoni usisite kututumia nasi tutafurahi kupokea maoni yako kuhusu vipindi hivi hadi wakati mwengine tutakapokutana nawe kwa makala nyingine ya ***Learning By Ear***, kutoka ***Bonn*** twakutakia kila la kheri katika shughuli zako za biashara!

<b>Music up</b>
-----------------

END